JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAELEZO MAFUPI KWA UMMA WA TANZANIA KUHUSU MPANGO WA NCHI ZA KIAFRIKA WA KUJIPIMA KWA KUTUMIA VIGEZO VYA UTAWALA BORA (AFRICAN PEER REVIEW MECHANISM – APRM)

UTANGULIZI:

1. Hivi karibuni serikali imeanzisha mchakato wa Kujipima kwa Kutumia Vigezo vya Utawala Bora, unaojulikana kwa Kiingereza kama "The African Peer Review Mechanism ama APRM" kwa kifupi. Madhumuni ya maelezo haya ni kuwawezesha wananchi kuufahamu vizuri mchakato huu na hivyo kuwawezesha kutoa mchango wao katika kufanikisha malengo ya zoezi hilo.

2. Chimbuko la APRM ni Mpango Mpya wa Maendeleo ya Afrika (New Partnership for Africa's Development-NEPAD), ambao unalenga kuliondoa bara la Afrika kutoka kwenye lindi la umaskini, na kuleta maendeleo. NEPAD imeunganisha mipango ya maendeleo iliyobuniwa chini ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika, (OAU), na kuainisha ukosekanaji wa utawala bora kama mojawapo ya vikwazo dhidi ya maendeleo yanayolikabili bara la Afrika. Hivyo, ili kukabiliana na kikwazo hiki, viongozi wa nchi za Umoja wa Afrika (UA) walitoa Tamko Kuhusu Demokrasia, Siasa, Uchumi na Uongozi Bora katika nyanja za uchumi na mashirika ya kibiashara. Tamko hilo pia linaainisha mkakati wa kufanikisha azma hii, kupitia demokrasia na utawala bora.

3. Mpango wa Kujipima kwa kutumia vigezo vya Utawala Bora ni mpango wa hiari, uliobuniwa na viongozi wa nchi za Umoja wa Afrika, kuziwezesha nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, kujitathmini katika utendaji wa shughuli za serikali na shughuli zao nyingine kwa ujumla. Aidha mpango huu unalenga kuzipa nchi wanachama, fursa ya kujifunza kutokana na uzoefu na mafanikio ya nchi zingine za Kiafrika, na hivyo kuziwezesha nchi husika kuiga sera na mbinu muafaka zilizoleta mafanikio hayo kwa manufaa ya nchi zao. Kwa ujumla, ombi la kufanyiwa tathmini linapofanywa, linaashiria nchi husika kukubali kufuata misingi ya utawala bora katika uendeshaji wa siasa na shughuli za kiuchumi na wakati huohuo, kukubali kufanyiwa tathmini na Viongozi Wenza wa nchi za Kiafrika. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipeleka maombi ya kujiunga na mpango huu tarehe 26 Mei, 2004 na kukubaliwa rasmi tarehe 8 Julai 2004, wakati wa Kikao cha Tano cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika.

4. Hadi sasa nchi 27 kati ya nchi 53 wanachama wa Umoja wa Afrika zimejiunga na mpango wa APRM. Mpango huo unahusisha uhakiki katika vipindi mbalimbali (periodic reviews) wa sera, kanuni na taratibu za utendaji zilizozoeleka (practice) ili kubaini maendeleo yaliyopatikana katika kutekeleza malengo yaliyokubaliwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na utawala wa pamoja wa kibiashara kama

ilivyoainishwa kwenye Tamko la Demokrasia, Siasa, Uchumi na Utawala wa Pamoja.

5. Licha ya Tanzania nchi zingine zinazoshiriki kwenye mchakato huu ni: Afrika ya Kusini, Algeria, Angola, Burkina Faso, Benin, Cameroon, Congo, Egypt, Ethiopia, Gabon, Ghana, Kenya, Lesotho, Mali, Malawi, Mauritius, Mozambique, Nigeria, Sao Tome na Principe, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Sudan, Uganda, Zambia na Djibouti. Kati ya nchi hizo, Ghana, Rwanda, Kenya na Afrika ya Kusini zimekwishafanyiwa tahmini, wakati nchi zilizobaki ziko katika hatua mbalimbali za kufanyiwa tathmini hizo. Lengo kuu la tathmini ni kubaini udhaifu uliopo nchini katika kutekeleza utawala bora na kutafuta njia za kukabiliana na udhaifu huo.

6. Dhana ya utawala bora kwa minajili ya APRM, ni pana na inahusisha sekta zote ambazo kwa namna moja au nyingine, zinagusa maslahi ya mwananchi. Hivyo, licha ya kuhusisha utendaji wa mihimili mitatu ya dola, hususan, Serikali, Bunge na Mahakama, tathmini itakayofanywa, pia itavijumuisha vyombo vya habari pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali, (ASIZE ama NGOs) ambazo zina dhima kubwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

UTARATIBU NA VYOMBO VITAKAVYOSIMAMIA MCHAKATO WA APRM

7. Mpango wa kujipima kwa kutumia Vigezo vya Utawala Bora una hatua tano muhimu, na unasimamiwa na Makao Makuu ya APRM, yaliyoko Afrika ya Kusini. Makao Makuu yaa APRM yana majukumu yafuatayo:

(i) Kuweka kumbukumbu za taarifa za maendeleo ya kisiasa na kiuchumi katika nchi zinazoshiriki katika mchakato wa kujipima;
(ii) Kutayarisha mada za msingi kuhusu nchi zinazofanyiwa tathmini kwa ajili ya matumizi ya Timu za Wataalam zinzotegemewa kufanya tathmini;
(iii) Kupendekeza vigezo vya utendaji na kufuatilia utendaji wa nchi mbalimbali zinazoshiriki katika mchakato wa APRM.

8. Katika hatua ya kwanza ya mchakato huu, nchi inajipima yenyewe, kuhusu inavyojiona kwenye kutekeleza utawala bora. Ili kukidhi malengo kulingana na vigezo vilivyopo, tathmini hii inatakiwa ifanywe na chombo kilichokuwa huru na kwa uwazi na ukweli. Nchini mwetu tathmini hii itafanywa na Sekretariati iliyoundwa mahsusi, kwa minajili ya kuratibu shughuli za APRM, chini ya Baraza la Usimamizi la Kitaifa, (National Governing Council).

9. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Kikwete amemteua Profesa Hasa Mlawa kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi la Kitaifa. Wajumbe wa Kamati hii ni kama ifuatavyo:

1. Profesa Hasa Mlawa - Mwenyekiti,
2. Bibi Thecla Shangali - Katibu, Tume ya Utumishi wa Umma,
3. Bw. Said M.Muhammed - Wizara ya Katiba na Utawala Bora, Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar,
4. Bw. Mathew Mhina Mwaimu - Wizara ya Katiba na Sheria 5. Bibi Rosemary Jairo - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,
6. Bw. Anthony Ngaiza - Baraza la Habari la Tanzania,

7. Profesa Ibrahim Shao - Taasisi ya Maendeleo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
8. Dr. Salim Nasser - Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo, Zanzibar (Zanzibar Chamber of Commerce, Industry and Agriculture),
9. Bw. Willigis Mbogoro- Muungano wa Vyama vya Ushirika Tanzania, (Tanzania Federation of Cooperatives),
10. Bw. Samson Chemponda- Baraza la Biashara la Tanzania (National Business Council),
11. Bw. Hassan Siraji Luambano - Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA)
12. Bi. Oliva Kinabo - Baraza la Maaskofu la Tanzania,
13. Bw. Nestory Masswe - Asasi Zisizo za Kiserikali (ASIZE) ama Tanzania Non-Governmental Organisation (TANGO),
14. Bw. Elvis Musiba - Tanzania Private Sector Foundation (TPSF),
15. Mh. Said Amour Arfi (Mb) – Bunge la Tanzania,
16. Mh. Dr. James Wanyancha (Mb.) – Bunge la Tanzania,
17. Bw. Palemon G. Rujwahula - Jumuiya ya Wasiojiweza,
18. Profesa Ruth Meena- Mtandao wa Jinsia Tanzania (Tanzania Gender Networking Programme - TGNP),
19. Bw. J.G. Wilson Mallya-Chama cha Wakulima Tanzania (Tanzania Farmers Association),
20. Bw. Peter Joseph Masika - Tanzania Youth Alliance (TAYOA).

10. Kati ya Wajumbe 20, wawakilishi 4 walioteuliwa wanatoka ama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wajumbe hawa wameteuliwa kutokana na nyadhifa wanazoshikilia na ni watendaji wanaohusika moja kwa moja na maswala ya utawala bora. Wajumbe waliobaki wamependekezwa na asasi mbalimbali za kiraia zilizo na maslahi kwenye utawala bora. Mh. Rais pia ameiteua Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwa kiungo kati ya Serikali na Makao Makuu ya APRM yenye Makao Makuu huko Afrika ya Kusini.

11. Aidha, serikali imeunda sekretarieti ya APRM Tanzania kama chombo kinachojitegemea, na chenye majukumu ya kuratibu ukusanyaji wa maoni ya wananchi juu ya utawala na kuyafanyia tathmini. Sekretarieti hiyo ya APRM Tanzania inaongozwa na Profesa Daudi Mukangara kama Katibu Mtendaji. Kabla ya uteuzi huu Profesa Mukangara alikuwa akifundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ofisi za Sekretarieti hiyo sasa hivi ziko katika ghorofa ya tano ya Jengo la Kitega Uchumi, Barabara ya Samora.

12. Katika kutekeleza majukumu yake, Sekretarieti hiyo itasaidiwa na Taasisi za Kitaalam (Technical Assessment Teams-TAT). TAT ndizo zitakazoshughulikia maeneo manne ya Mchakato wa APRM hususan, Demokrasia na Utawala Bora katika nyanja za Kisiasa; Utawala Bora katika Uchumi; Uendeshaji Bora wa Mashirika ya Kibiashara; na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi. Kwa ushauri wa Sekretarieti ya APRM, Baraza la Usimamizi la Kitaifa limeteua asasi za kitaalam zitakazosaidiana na Sekretarieti kufanya tathmini. Taaasisi zilizochaguliwa ni kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye eneo la Demokrasia na Utawala Bora Kisiasa.
(b) Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye eneo la

Utawala Bora Kiuchumi.

(c) Research on Poverty Alleviation (REPOA) kwenye eneo la Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi.
(d) Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii kwenye Uendeshaji Bora wa Mashirika ya Kibiashara.

13. Katika kukusanya maoni ya wananchi kuhusu utendaji na uwajibikaji wa Serikali yao na utawala bora kwa ujumla, Taasisi za Kitaalam zitaongozwa na maswali yaliyo katika hojaji, kwa kutumia njia za kawaida za utafiti, hususan utafiti kwenye maktaba, uchunguzi wa sera, mipango na programu za serikali, pamoja na mahojiano ya ana kwa ana na wananchi mmoja mmoja, ama kupitia vikundi,kuuliza maswali hayo hayo kwa wataalam pamoja na kutumia utaalam na uzoefu wa watafiti ili kupata majibu ya hojaji. Aidha njia zingine zitakazotumiwa, ni kwa kupitia vipindi vya redio na televisheni na matangazo ya magazetini, pamoja na kupokea maoni kwa njia ya barua pepe.

HATUA ZA MCHAKATO WA TATHMINI:

14. Mchakato wa APRM una hatua tano muhimu. Hatua ya kwanza inahusu uchunguzi na tathimini katika maeneo manne ya:

(i) Demokrasia na Utawala Bora Kisiasa;
(ii) Utawala Bora Kiuchumi;
(iii) Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi; na
(iv) Uendeshaji Bora katika Mashirika ya Kibiashara.

Baada ya kupokea na kutathmini maoni ya wananchi na utafiti wa kitaalam, Sekretariati ya APRM itatayarisha taarifa kuhusu hali ya utawala bora ilivyo nchini. Itajadiliwa na wadau mbalimbali nchini, kabla ya kuwasilishwa Makao Makuu ya APRM. Licha ya kuelezea mapungufu yatakayojitokeza, taarifa hiyo pia inatakiwa kutayarisha mpango wa jinsi ya kuyakabili mapungufu hayo (Plan of Action-PoA), kabla ya kuiwasilisha taarifa hiyo kwenye Sekretariati ya APRM ngazi ya Bara la Afrika iliyopo Afrika ya Kusini. Wakati huo huo Makao Makuu ya APRM yatakuwa yametayarisha Taarifa ya Awali kuhusu Tanzania kutokana na mada mbali mbali zilizokwisha andikwa na wangine huko nyuma.

15. Katika awamu ya pili ujumbe kutoka Makao Makuu ya APRM huko Afrika ya Kusini, hutembelea nchi inayofanyiwa tathmini, ili kuhakiki kama zoezi la kujipima limefanywa kwa uwazi na ukweli kama inavyotegemewa. Ujumbe huu unajumuisha Wataalam wa Kiafrika waadilifu, na wenye utumishi uliotukuka katika fani zinazohusiana na shughuli za APRM na dhamira ya kuleta Umoja wa Afrika (Pan-Africanism). Wajumbe hao huchaguliwa kutokana na jopo lenye kati ya wataalam watano hadi saba, wanaochaguliwa kutoka jinsia zote, na kuwakilisha kanda zote za Bara la Afrika.

16. Kwa upande wa nchi yetu, Profesa Adebayo Adedeji, aliyewahi kuwa Katibu Mwendeshaji wa Ofisi ya Kanda ya Afrika ya Umoja wa Mataifa (UNECA) iliyoko Addis Ababa, ameteuliwa kusimamia mchakato wa APRM kwa Tanzania na ndiye atakayeongoza Ujumbe wa Wataalam kutoka Makao Makuu ya APRM. Katika kutekeleza majukumu yake, Profesa Adedeji alitembelea Tanzania tarehe 6 hadi 8 Juni, 2006 ili kushauriana na serikali yetu jinsi ya kujipanga katika kutekeleza zoezi

la kujipima.

17. Profesa Adedeji atakuwa na jukumu la kusimamia zoezi la nchi kujitathmini, hususan kujiridhisha kwamba mchakato wa APRM umeendeshwa kwa uwazi na ukweli. Wakati wa ziara hiyo, Ujumbe kutoka Makao Makuu ya APRM, utatoa kipaumbele kwa shughuli ya kufanya mashauriano na serikali, watumishi wa serikali, vyama vya kisiasa, Wabunge na wawakilishi wa Asasi Ziziso za Kiserikali, zikiwemo vyombo vya habari, wasomi, vyama vya wafanyakazi, na vyama vya wataalam, (professional bodies), na wafanyabiashara.

18. Awamu ya tatu inahusu utayarishaji wa taarifa ya Ujumbe uliofanya tathmini. Taarifa hii itatayarishwa kwa misingi ya mada zilizoandaliwa na Makao Makuu ya APRM, Sekretarieti, pamoja na maelezo yaliyotolewa nchini kutoka vyanzo vya Kiserikali na visivyo vya Kiserikali, wakati wa mashauriano na wadau mbalimbali.

19. Taarifa ya timu ya APRM inatakiwa kuwa ya uwazi na ukweli na kuonyesha kinagaubaga, mapungufu yatakayobainika. Hususan, taarifa inatakiwa kulenga kuelezea endapo kuna utashi kwa upande wa Serikali wa kuchukua hatua na kurekebisha mapungufu yaliyobainika na itahitaji muda gani kufanya hivyo. Je, nyenzo ama rasilimali gani itahitaji kurekebisha mapungufu? Kati ya rasilimali inayohitajika, kiasi gani kinaweza kugharamiwa na Serikali yenyewe na kiasi gani kinahitajika kupatikana kutoka vyanzo ambavyo viko nje ya Serikali? Kama uwezo utapatikana, itachukua muda gani kurekebisha mapungufu yaliyobainika?

20. Rasimu ya taarifa hiyo itajadiliwa kwanza na Serikali. Lengo la mjadala huu ni kuhakiki usahihi wa taarifa iliyotolewa, na kuipa serikali nafasi ya kujibu hoja zilizomo katika taarifa na kutoa mapendekezo yake juu ya kukabiliana na mapungufu yatakayokuwa yamejitokeza. Hata hivyo, majibu ya serikali hayawezi kubadilisha taarifa ya Wataalam wa APRM ila majibu hayo, yataambatanishwa na taarifa ya Tume ya Wataalam wakati taarifa itakapowasilishwa mbele ya Wakuu wa Nchi Wenza.

21. Katika hatua ya nne Makao Makuu ya APRM, yanawasilisha taarifa ya tathmini yake mbele ya Wakuu wa Nchi Wenza (Peers) wa nchi zinazoshiriki katika mchakato wa APRM, kwa majadiliano, na mapendekezo ya Wakuu wa Nchi Wenza. Maamuzi na mapendekezo yatakayochukuliwa na Viongozi Wenza yatategemea utashi wa nchi inayofanyiwa tathmini. Serikali husika inapoonyesha nia ya dhati ya kushughulikia mapungufu yaliyojitokeza, nchi zinazohusika na mchakato huu zina wajibu wa kuisaidia nchi inayotathminiwa, kulingana na uwezo wao, ikiwa ni pamoja na kuziomba nchi wahisani na asasi za kimataifa kutoa msaada unaohitajika.

22. Pale inapodhihirika kwamba nchi husika haina dhamira ya kushughulikia mapungufu, Viongozi Wenza hujaribu kuishawishi nchi hiyo kushughulikia mapungufu yaliyobainika, kwa njia ya majadiliano na ahadi za misaada. Kama majadiliano haya hayatazaa matunda, basi kama hatua za mwisho baada ya mazungumzo kushindikana, Wakuu wa Nchi wanaweza kuipatia nchi husika notisi juu ya dhamira ya pamoja ya viongozi hao kuichukulia nchi hiyo hatua na kuipa tarehe ya kikomo ya kushughulikia mapungufu. Kipindi hiki kitatoa nafasi kwa nchi husika kushughulikia mapungufu yaliyobainishwa, kwa njia ya mjadala.

23. Zoezi la kujipima litahitimishwa kwa taarifa ya tathmini kufikishwa mbele ya

asasi za Umoja wa Afrika, hususan Bunge, Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu, Baraza la Amani na Usalama na Baraza la Uchumi, Maswala ya Kijamii na Kiutamaduni, (ECOSOCC). Hii ndiyo hatua ya mwisho ya mchakato wa tathmini, na inatakiwa ichukuliwe miezi sita baada ya Wakuu wa Nchi kuipokea na kuijdadili taarifa husika.

24. Gharama za APRM zinabebwa kutokana na michango ya nchi wanachama. Zoezi la tathmini litafanywa mara moja kila baada ya miaka mitano. Zoezi lote la mchakato wa APRM linatakiwa lichukue muda wa miezi 9 hadi 12 kuanzia hatua ya kwanza hadi taarifa kuwasilishwa mbele ya Wakuu wa Nchi.

HITIMISHO

25. Tanzania imejiunga na mchakato huu kupitia serikali yake, kwa hiari yake yenyewe na kwa nia njema ya kupanua wigo wa demokrasia, na kuwapa wananchi kauli katika maamuzi yanayohusu mustakabali ya nchi yao. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inategemea kuwa wananchi watatumia kikamilifu, nafasi iliyotolewa ili kutoa tathmini yao ya kweli, kuhusu yale wanayoyaona kuwa ni mapungufu ya utendaji serikalini na mapungufu ya utawala bora nchini kwa ujumla, ili kuiwezesha serikali nayo kuyabaini mapungufu hayo na kuyachukulia hatua muafaka. Ni kwa kufanya hivyo ndipo malengo ya zoezi hili yatakapotekelezwa.

26. Ili kukidhi matarajio yaliyokusudiwa, Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania inataraji kuendesha tathmini ya utendaji wake na vyombo vyake kwa uwazi, ukweli na umakini, kulingana na vigezo vilivyowekwa kwenye Mpango wa Kujipima kwa kutumia Vigezo vya Utawala Bora.

27. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inategemea kuwa kushiriki kwake katika mchakato wa APRM utapanua wigo wa demokrasia, na kuwapatia wananchi fursa nyingine ya kuelezea dukuduku zao juu ya utendaji wa serikali yao, na hivyo kuchangia katika kudumisha utengamano, kuleta maendeleo pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kikanda kwa njia ya kubadilishana uzoefu na kuiga mifano bora ikiwa ni pamoja na kutambua udhaifu na kutathmini mahitaji ya kuongeza uwezo wa serikali na nchi.

28. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaamini kuwa zoezi la kujitathmini na kujitambua, litatoa chachu kwa nchi kufikiria kwa makini sera za ndani, si tu katika kuchangia utengamano wa kisiasa (political stability), na ukuaji wa uchumi, bali hata kwa nchi jirani. Aidha itasaidia katika kuleta manufaa ya kuwajibika kwa pande zote (mutual accountability) na kutekeleza/kutimiza/kufuata mambo bora (best practices). Hivyo shime wananchi, shirikianeni na Baraza la Usimamizi na Sekretarieti ya APRM, kwa kutoa mawazo yenu bila woga ili tujenge mustakabali wa pamoja kuhusu nchi yetu na kutimiza kikamilifu malengo ya zoezi hili.

Imetolewa na
KATIBU MKUU
WIZARA YA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA